JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAISI

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI, MTAMBULA

S.L.P 407,

MAFINGA

Kumb Na: MTASS US/KI/VOL.1/16

JINA LA MWANAFUNZI.

……

……

YAH**:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MTAMBULA**

01.UTANGULIZI

Napenda kuchukua fulsa hii kukupa pongezi kwa kuchaguliwa na kujiunga na shule hii , shule ipo katika kijiji cha **Mtambula-kata ya Mtambula tarafa ya Kasanga wilaya ya Mufindi mkoa wa Iringa.**

02.KUFUNGUA SHULE

Shule itafungua tarehe 11/01/2021 na kila mwanafunzi atatakiwa afike shuleni siku ya kufungua shule bila kukosa, akiwa na mahitaji yote kama ilivyoagizwa .Shule ni ya kutwa na ni mchanganyiko.

03.MASOMO

Shule inafundisha masomo yafuatayo;

HISABATI, JIOGRAFIA, KISWAHILI, URAIA, KIINGEREZA, BAIOLOJIA, KEMIA, FIZIKIA, HISTORIA na somo la dini kila mwanafunzi atahudhuria vipindi vya dhehebu lake. Masomo yote yatafundishwa kwa kiingereza isipokuwa somo la dini na Kiswahili .

04. SARE YA SHULE NA VIFAA MUHIMU KWA MWANAFUNZI

A. SARE YA SHULE KWA WAVULANA

- Suruali moja rangi ya maroon au damu ya mzee
- Suruali moja dark blue .(blue nyeusi)
- Shati nyeupe tetron mbili mikono mirefu
- Tai mbili, damu ya mzee (01) na dark blue (01)
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili (02) vyenye kamba (buti hairuhusiwi)

- Soksi jozi mbili rangi nyeusi.
- Sweta 2 moja rangi ya damu ya mzee na jingine dark blue.
- Nguo za michezo (fulana bukta na raba) pia awe na tracksuit nyeusi ambayo huvaliwa Jumatano na siku za michezo.
- Kitambaa kwa ajili ya makamasi (lesso)

B.SARE YA SHULE KWA WASICHANA

- Sweta 2 moja rangi ya damu ya mzee na jingine dark blue
- Sketi moja rangi ya damu ya mzee kitambaa kizito linda box.
- Sket moja rangi ya dark blue,kitambaa kizito linda box.
- Blauzi mbili nyeupe tetroni mikono mirefu.
- Tai mbili, damu ya mzee moja na dark blue moja.
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili .
- Nguo za michezo (fulana ,bukta na raba)na tracksuit nyeusi ambayo huvaliwa ijumaa na siku ya michezo.
- Soksi jozi mbili rangi nyeupe
- Kitambaa kwa ajili ya makamasi (lesso)
  .

05.VIFAA VINGINE VINAVYOHITAJIKA SHULENI

- Faili jipya la plastiki kwa ajili ya kuhifadhia kumbukumbu mbalimbali za mwanafunzi.
- Mchango wa chakula mahindi debe moja yaliyo kobolewa (nusu muhula), maharage lita nane.
- Sahani ya chakula ya plastic rangi nyekundu

06.VIFAA BINAFSI VINAVYO HITAJIKA MWANAFUNZI AWE NAVYO

- Mkebe wenye vifaa vyote (mathematical set)
- Dictionary (kamusi ya kiingereza).
- Daftari aina ya counter books kumi (2 QUIRE)

07.MAELEZO MENGINE MUHIMU

- Inasisitizwa kwa kila mwanafunzi aje na mahitaji muhimu ili kuepusha usumbufu
- Kila mwanafunzi atalazimika kutii na kuheshimu sheria zote za shule na taratibu zake .(sheria za shule zimeambatanishwa).
- Kila mwanafunzi itamlazimu kujifunza na kujua wimbo wa Taifa, nyimbo za kizalendo na wimbo wa shule.
- Kila mzazi/mlezi na mwanafunzi husika inamlazimu kujaza kiambatisho ‘A’ na ‘B’ kwa ukamilifu na kuleta shuleni mnamo tarehe 11/01/2021
- Simu haziruhusiwi shuleni,ukipatikana nayo utafukuzwa shule.
- Unashauriwa kumtafutia mwanao cheti cha kuzaliwa,ni muhimu sana na aje nacho kikiwa ndani ya faili.
- Unatakiwa kumleta mwanao siku ya kufungua shule ,ifikapo tarehe; 11/01/2021 iwapo hujamleta mwanao,hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yako.
  NB; MWANAO ASIPO FIKA SHULENI KUANZIA HIYO TAREHE ATAHESABIKA KUWA NI MTORO

08.SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

9.1. Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa **Sheria ya Elimu Na 25 Mwaka 1978,** aidha inazingatia mambo ya msingi yafuatayo , ambayo yatafafanuliwa kwako mara ufikapo shuleni.

a) Heshima kwa viongozi ,walezi,wafanyakazi wote,na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote uwapo shuleni au safarini.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Huruhusiwi kumiliki SIMU AU RADIO uwapo katika mazingira ya shule
j) Huruhusiwi kuvaa kofia au gloves uwapo katika mazingira ya shule.
k) Sare ya shule kwa wavulana (suruali) itavaliwa na mkanda mweusi wa ngozi
l) Suruali ishonwe ikiwa na malinda na turn up,modo na mshono wa jeans hautaruhusiwa.

9.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.

1. wizi

2. Uashereti,ubakaji na ushoga

3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya

4 Uvutaji bangi,unga na sigara

5. Makosa ya jinai

6 .Kupigana na kupiga

7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma au mwanafunzi mwenzako.

8. Kudharau bendera ya taifa

9. Kuoa au kuolewa

10. Kupata mimba au kusababisha mimba.

11. Kutoa mimba

12. kugoma , kuchochea au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

13.Kukataa kwa makusudi adhabu uliyopewa na mwalimu.

9.3 MAMBO MENGINE MUHIMU

Kila mzazi/mlezi ahakikishe anafanya yafuatayo.

- kumpeleka mtoto wako hospitali ili akapimwe afya (tumia fomu kitambulisho 'A')
- fomu ya maelezo binafsi historia ya mwanafunzi .(tumia fomu kitambulisho 'B')

- kuwasilisha fomu zote mbili yaani fomu A na B ,zikiwa zimejazwa kikamilifu na ziwe ndani ya faili cover aina ya folder file .(kama ilivyoagizwa hapo juu).
- Kufuatilia maendeleo ya mtoto wako mara kwa mara, na ujiridhishe anafika shuleni.

NB; TAFADHARI SOMA KWA MAKINI MAELEZO /MAAGIZO HAYO YOTE NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU, ILI KUEPUKA USUMBUFU USIO WA LAZIMA. KWANI KWA MUJIBU WA <u>SERIKALI</u> KUMLETA MTOTO WAKO SHULENI NI LAZIMA SIO OMBI.

.....

OMARI R. MAGAA

MKUU WA SHULE

Nakala:

MKURUGENZI MTENDAJI (W),

S.L.P 223,

MAFINGA.

AFISA ELIMU (W),

S.L.P 214

MAFINGA.

AFISA MTENDAJI KATA MTAMBULA

S.L.P

MAFINGA